**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA**

Unapojibu tafadhali taja

Kumb.Na.DED/S.20/5/ VOL. IV/135 Tarehe: 23/05/2022

# Yah: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa ya kujaza nafasi mbalimbali za kazi zifuatazo;

**1.0. NAFASI: MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III (Nafasi 12)**

**1.1. SIFA ZA MWOMBAJI**

Mwombaji anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

(a) Mwenye elimu ya kidato cha nne (Form IV) au kidato cha sita (Form VI)

(b) Awe na Astashahada / **Cheti NTA level 5** katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii, Mipango na Sayansi ya Siasa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**1.2. MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA III**

Mwombaji atakayefaulu na kuajiriwa atatekeleza majukumu yafuatayo:

(a) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji

(b) Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao na kuwa Mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji.

(c) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezajiwa mipango ya maendeleo ya Kijiji.

(d) Katibu wa mikutano/Vikao na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.

(e) Kutafsiri na kusimamia sera, kanuni, taratibu na Sheria za Nchi.

(f) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali pamoja na kipato binafsi.

(g) Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika Kijiji.

(h) Kusimamia, kukusanya na kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.

(i) Mwenyekiti wa Vikao vyote vya wataalamu katika Kijiji.

(j) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi.

(k) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo ndogo za Kijiji.

(l) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

**1.3. MSHAHARA**

Kwa kuzingatia Muundo na ngazi za Mshahara ya Watumishi wa Serikali yaani TGS B/1 kwa mwezi.

**2.0 KATIBU MAHUSUSI DARAJA III ( Nafasi 4)**

**2.1. SIFA ZA MWOMBAJI**

a) Mwenye elimu ya kidato cha nne (Form IV) au kidato cha sita (Form VI

b) Awe na Astashahada / Cheti **NTA level 5** cha mafunzo ya uhazili na Kufaulu Mtihani wa hatua ya Tatu. Awe wamefaulu somo la Hati Mkato ya Kiswahili na Kiingereza Maneno **80** kwa dakika moja na awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali .

**2.2 MSHAHARA**

Kwa kuzingatia Muundo na ngazi za Mshahara ya Watumishi wa Serikali yaani TGSB/1 kwa mwezi.

**3.0 MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA II (Nafasi 4)**

**3 .1. SIFA ZA MWOMBAJI**

a) Mwenye elimu ya kidato cha nne (Form IV) au kidato cha sita (Form VI
b) Awe na Astashahada / Cheti **NTA level 5** cha utunzaji Kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya na Masjala

**3.2 MSHAHARA**

Kwa kuzingatia Muundo na ngazi za Mshahara ya Watumishi wa Serikali yaani TGS B/1 kwa mwezi.

**4.0 DEREVA DARAJA LA II (Nafasi 3)**

**4 .1. SIFA ZA MWOMBAJI**

a) Mwenye elimu ya kidato cha nne (Form IV) au kidato cha sita (Form VI
b) Awe na Cheti cha Mafunzo ya msingi (Basic Driving Course) kinachotolewa na Chuo cha Mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine chochote kinachotambuliwa na serikali. Muombaji mwenye cheti cha Majaribio ya Ufundi daraja la II atafikiriwa kwanza.

**4.2 MSHAHARA**

Kwa kuzingatia Muundo na ngazi za Mshahara ya Watumishi wa Serikali yaani TGS B/1 kwa mwezi

**5. MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI**

(a) Mwombaji awe ni raia wa Tanzania.

(b) Awe na umri kuanzia miaka **18** na asiyezidi miaka **45.**

(c) Awe Mtanzania mwenye akili timamu.

(d) Maombi yote yaambatane na vivuli (photocopies) vya vyeti vya Taaluma, Ujuzi, cheti cha kuzaliwa, picha mbili (2) (Passport size) za rangi za hivi karibuni.

(e) Waombaji wote waambatanishe Wasifu wenye maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV), yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina matatu ya wadhamini (Referees) wa kuaminika.

(f) Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinahakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (**TCU, NECTA na NACTE**).

(g) Maombi yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

(h) Waombaji wa kazi ambao tayari ni waajiriwa katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyopo katika Waraka Na. **CAC.45/257/01/D//140** wa tarehe **30/11/2020**.

(i) Waombaji waliostaafu Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

(j) Awe hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai.

(k) ''Testimonial'' ''Provisional Results'' ''Statement of Results'' hati ya matokeo ya kidato cha nne au sita (Form IV and Form VI) "Results Slips" HAVITAKUBALIWA.

(l) Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria.

(m) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 06/06/2022 saa 9:30 Alasiri

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Songea,
1barabara ya Halmashauri,
S.L.P. 995,
**57183 SONGEA, RUVUMA.**

Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Halmashauri ambayo ni www.songeadc.go.tz na tovuti ya Sekretarieti ya Ajira/Ajira portal....

Imetolewa na,

Neema M. Maghembe
MKURUGENZI MTENDAJI (W),
**SONGEA.**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
SONGEA